# NAFASI ZA KAZI

TTCL Corporation

## WAKALA WA USAJILI HUDUMA YA FAIBA

Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) linawatangazia Vijana wenye sifa na uwezo wa kufanya kazi ya kuwa Wakala wa Usajili wa Huduma ya Faiba katika Mikoa ya **Mbeya, Iringa, Dodoma** na **Mwanza.**

### 1. SIFA ZA MUOMBAJI

Muombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- Umri usiopungua miaka 18.
- Awe raia wa Tanzania mwenye Kitambulisho halali cha Taifa (NIDA) au Kitambulisho cha Mpiga Kura au Leseni ya Udereva.
- Awe na cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne.
- Awe anaishi katika Mkoa husika.
- Awe na uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili na/au Kiingereza.
- Awe na nidhamu, uadilifu, na asiwe na rekodi ya makosa yoyote ya jinai au mashtaka yanayohusiana na uaminifu.
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja (smartphone).
- Awe tayari kupokea mafunzo na kufuata miongozo ya Shirika.
- Awe na uwezo wa kujieleza na kuwasiliana na wateja.

### 2. RATIBA NA MAHALI PA USAHILI

| JINA LA MKOA | TAREHE | MUDA | ENEO |
|---|---|---|---|
| MBEYA | 20 Januari, 2026 | Saa 3:00 asubuhi | Ofisi za TTCL Mkoa wa Mbeya • Mtaa wa Maktaba |
| IRINGA | 25 Januari, 2026 | Saa 3:00 asubuhi | Ofisi za TTCL Mkoa wa Iringa • Mtaa wa Posta |
| DODOMA | 30 Januari, 2026 | Saa 3:00 asubuhi | Ofisi za TTCL Mkoa wa Dodoma • Mtaa wa Posta |
| MWANZA | 04 Februari, 2026 | Saa 3:00 asubuhi | Ofisi za TTCL Mkoa wa Mwanza • Mtaa wa Posta Nyamagana |

### 3. TARATIBU ZA MAOMBI

- Waombaji wote wanatakiwa kufika katika Ofisi za TTCL za Mkoa husika kulingana na ratiba hapo juu. Waombaji wafike na nakala ya Cheti na kitambulisho halali.

Kwa taarifa zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia **0222 100 100** au barua pepe: **barua@ttcl.co.tz**

@ttcl_Corporation